# HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO NA USHIRIKA MHESHIMIWA PAUL P. KIMITI (MBUNGE) WAKATI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 1997/98

## I. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kujadili na hatimaye kuidhinisha makadirio ya Wizara ya Kilimo na Ushirika kwa mwaka 1997/98.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kutumia nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala (Mbunge), kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri wa Kilimo na Ushirika. Pia napenda kumpongeza Katibu Mkuu Luteni Kanali Tirumanywa Philibert Magere kwa kuteuliwa kushika wadhifa huu katika Wizara yangu. Ningependa kutumia nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wapya waliochaguliwa katika kipindi hiki na kutoa rambirambi na pole zangu kwa wale wote tuliowapoteza katika Bunge letu kwa njia moja au nyingine.

3. Mheshimiwa Spika, sasa napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Frederick T. Sumaye (Mbunge) kwa hotuba yake nzuri ambayo imefafanua masuala mengi ya sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na Sekta ya Kilimo, Mifugo na Ushirika. Aidha napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri wenzangu wawili walionitangulia kwa hotuba zao ambazo zimefafanua masuala mengi ya kiuchumi na kijamii. Vilevile nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao ambayo imesaidia sana kuonyesha maeneo yanayohitaji msisitizo katika Wizara yangu. Kwa kweli mengi mliyoyazungumza katika Wizara hizo, yamenisaidia hasa katika kuimarisha maandalizi ya utekelezaji wa mipango ya Wizara yangu. Nawashukuru tena kwa hilo.

### Hali ya Chakula Duniani

4. Mheshimiwa Spika, kila mwaka Wizara yangu huwa inatoa taarifa fupi juu ya hali ya chakula duniani. Taarifa hii ni muhimu kwa sababu inatusaidia kujizatiti zaidi katika matumizi ya chakula chetu. Kufuatana na taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) ya Aprili, 1997 uzalishaji wa nafaka duniani katika kipindi cha 1996/97 unatarajiwa kukidhi mahitaji na pengine kuwa na ziada kidogo. Makisio ya awali yanaonyesha uzalishaji wa tani 1,880 milioni ikilinganishwa na mahitaji ya tani 1,833 milioni kwa mwaka 1997/98.

5. Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo hali ya kujitosheleza kwa chakula

duniani, zaidi ya nchi 26, nyingi zikiwa katika Bara la Afrika ikiwemo Tanzania zitakabiliwa na upungufu mkubwa wa chakula na hivyo kuhitaji chakula cha msaada. Inakisiwa kwamba kiasi cha tani 7.5 milioni za chakula cha msaada zitahitajika ili kukidhi mahitaji ya chakula ya nchi hizo. Wakati mahitaji ya chakula cha msaada yanaonyesha ongezeko, upatikanaji wake umekuwa ukipungua mwaka hadi mwaka. Taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa ya mwaka 1997 inaonyesha kuwa upatikanaji wa chakula cha msaada umekuwa wa chini mno kuliko wakati mwingine wowote katika kipindi cha miaka ishirini iliyopita. Aidha kutokana na ongezeko kubwa la bei ya nafaka kwenye soko la dunia, nchi maskini zitashindwa kuagiza chakula cha nyongeza kutoka nje. Suala la upitikanaji wa chakula lilijadiliwa kwa kirefu katika Mkutano wa Nchi Wanachama wa FAO uliofanyika Rome, Italia Novemba 1996. Mkutano huo vile vile ulikubaliana na kuweka mihadi kwamba kila nchi ijitahidi kuwa na amani na utulivu, itumie rasilimali zake kwa uangalifu, juhudi ziwekwe katika kuongeza uzalishaji katika sekta za kilimo (husasan chakula), misitu na uvuvi. Aidha masuala ya kuondoa umaskini na kujiweka tayari kukabili na kudhibiti maafa yazingatiwe.

6. Mheshimiwa Spika, katika Bara la Afrika uzalishaji wa nafaka katika msimu wa 1996/97 unatarajiwa kuwa wa kuridhisha katika nchi za SADC zikiwemo Botswana, Lesotho, Namibia, Swaziland, Afrika Kusini na Zambia. Katika nchi hizo uzalishaji wa mahindi unakisiwa kufikia tani 20.5 milioni karibu sawa na msimu uliopita. Nchi za Malawi, Msumbiji na Zimbabwe zitapata mavuno pungufu kidogo kwa sababu ya mafuriko wakati Tanzania inakabiliwa na upungufu mkubwa wa uzalishaji wa mahindi kutokana na ukame. Katika nchi za Afrika Kaskazini Magharibi, hali ya uzalishaji wa chakula pia hairidhishi. Nchi za Cape Verde, Chad, Mauritania, Liberia na Siera Leone zimepata mavuno chini ya wastani. Wakati huo huo nchi za Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa chakula na kushindwa kuzalisha kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Katika nchi za Afrika Mashariki, hali ya chakula ni mbaya kutokana na kukosa mvua za vuli. Sehemu za Kaskazini Mashariki ya Kenya, mikoa ya Kusini ya Ethiopia nazo zinakabiliwa na tatizo hili. Aidha sehemu za Uganda na Ethiopia na Kaskazini ya Tanzania wananchi wengi hawana chakula cha kutosha.

**Hali ya Mazao ya biashara**

7. Mheshimiwa Spika, imethibitika kuwa bei ya mazao ya biashara yaliyoingizwa kwenye mfumo wa soko huria hutegemea sana bei ya soko la dunia. Kwa mara ya kwanza katika kipindi hiki tangu tuanze mfumo wa soko huru, bei katika soko la dunia kwa mazao ya korosho, kahawa, pamba na tumbaku, zilishuka kutoka viwango vya bei za soko hilo la nje za miaka ya 1994/95 na 1995/96. Hali hiyo imeyafanya mazao haya kupata bei za wakulima pungufu. Baadhi ya bei, zilipanda kidogo sana ikilinganishwa na bei ambazo wakulima wa mazao haya walizipata katika misimu iliyopita.

## II MAPITIO YA MWAKA 1996/97

### Mazao ya Chakula

8. Mheshimiwa Spika, kwetu sisi wakulima na wafugaji, mwaka huu wa fedha ulianza vibaya kama sote tunavyoelewa kuwa hali ya hewa kwa msimu wa 1996/97 hapa nchini haikuwa ya kuridhisha kutokana na ukame uliosababishwa na uhaba wa mvua na vipindi virefu vya jua. Uzalishaji wa mazao makuu ya chakula yakiwemo mahindi, uwele, mpunga, ngano, maharage, mihogo unatarajiwa kushuka ikilinganishwa na msimu uliopita. Makisio ya awali yanaonyesha kuwa uzalishaji wa chakula kwa jumla katika kipindi cha mwaka 1996/97 utashuka kwa asilimia 13.7 hadi kufikia tani 6.505 milioni ikilinganishwa na msimu uliopita ambao tulipata tani 7.498 milioni. Sababu kubwa zilizochangia katika kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula ni pamoja na:

(a) Kukosekana kwa mvua za vuli ambazo huchangia kwa wastani wa asilimia 30 ya uzalishaji wa chakula katika maeneo yanayopata mvua hizi.
(b) Kuchelewa kwa mvua za masika.
(c) Kupungua kwa maeneo yaliyolimwa nafaka wakati hasa wa msimu wa vuli.
(d) Matukio ya mafuriko katika baadhi ya maeneo nchini.
(e) Matumizi madogo ya mbolea kutokana na bei kubwa.

9. Mheshimiwa Spika, mahitaji yetu ya chakula kwa mwaka 1997/98 yanakisiwa kuwa tani 4.452 milioni kwa mazao ya nafaka na tani 2.682 milioni kwa mazao yasiyo nafaka. Hii ni jumla ya tani 7.134 milioni za chakula. Makisio ya mavuno ya awali kutokana na tathmini ya hali ya chakula nchini, iliyofanywa na Wizara ya Kilimo na Ushirika kwa kushirikiana na Idara Kuu ya Hali ya Hewa, Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Shirika la Chakula Duniani (WFP) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Amerika (USAID) mwezi Machi, 1997 imeonyesha pengo la tani 629,000 za mahitaji ya kitaifa. Pengo hili linapungua hadi tani 523,000 baada ya kufidiwa na mazao yasiyo nafaka, vyakula vyote vikichukuliwa maanani. Pengo hilo halina budi kuzibwa kwa kuagiza chakula kutoka nje ya nchi na ikibidi Serikali haitasita kuomba chakula cha msaada. Hata hivyo, kutokana na mvua ambazo licha ya kuchelewa kunyesha ziliendelea vizuri, Serikali ilitoa mbegu za muda mfupi kwa wakulima wa mikoa ya Pwani, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro na Arusha. Kwa kuwa wakulima waliitikia vizuri, pengo la upatikanaji wa chakula nchini halina budi kupungua. Hali halisi itajulikana baada ya kufanyika makisio ya mwisho ifikapo mwishoni mwa mwezi Julai, 1997.

### Mazao ya Biashara

10. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mazao ya biashara uzalishaji ulikuwa sio wa kuridhisha katika msimu wa 1996/97 ikilinganishwa na msimu wa 1995/96 kutokana na ukame. Uzalishaji wa kahawa ulipungua kwa asilimia 24, korosho kwa asilimia 19, chai kwa asilimia 20, pareto kwa asilimia 60 na mkonge kwa asilimia

31. Kwa upande wa pamba kumekuwa na ongezeko kidogo la asilimia 0.5 kutokana na kutokuwepo kwa bei ya kuvutia kwa wakulima. Kulikuwa na ongezeko kwa upande wa tumbaku kwa asilimia 25 kutokana na huduma nzuri za kuwapatia wakulima pembejeo kwa wakati unaotakiwa kwa njia ya kuwakopesha. Uzalishaji wa sukari uliongezeka kwa asilimia 2.6. Wizara yangu itaendelea kuwashauri na kuwahimiza wanunuzi wa mazao mbalimbali ya biashara kupeleka pembejeo za kutosha ili wakulima wazipate kwa wakati muafaka.

**Mazao yasiyo Asilia**

11. Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 1996/97 mazao ya mbegu za mafuta kama ufuta, mawese, nyonyo na soya yamepata msukumo mkubwa wa uzalishaji na utafiti. Shughuli hizi zimeendelea kuimarishwa katika kituo cha utafiti cha Naliendele - Mtwara. Vile vile mazao ya mboga, matunda, maua na viungo yameendelea kuhimizwa na yameonyesha kuwa na soko la ndani na nje ya nchi. Kwa mfano katika msimu wa 1996/97 kiasi cha tani 3,552 za mboga, maua, mbegu za maua, viungo na matunda ziliuzwa nchi za nje na kulileteа Taifa kiasi cha shilingi 2.7 bilioni. Kazi kubwa ambayo Wizara yangu inabidi iliwekee mkazo zaidi, ni upatikanaji wa soko la uhakika kwa wakulima wa mazao hayo. Pia Wizara itaweka msukumo maalum wa kuwahamasisha wawekezaji na kuandaa vivutio maalum kwa kuwataka waongeze vinu vya kusindika mafuta ili pamoja na kuandaa masoko yenye uhakika, mbinu bora za uzalishaji ziandaliwe ili wakulima wasione bughudha kwa kuyalima mazao hayo.

**Mazao Yatokanayo na Mifugo**

12. Mheshimiwa Spika, hali ya uzalishaji wa mazao yatokanayo na mifugo kwa kipindi cha mwaka 1996/97 kwa ujumla haikuwa nzuri hasa kutokana na maeneo mengi ya nchi kutopata kabisa mvua za vuli. Inakadiriwa kuwa karibu mifugo milioni 7 ilikabiliwa na tatizo kubwa la ukame hasa katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Mara, Mwanza na Tabora. Kutokana na hali hii, wafugaji katika mikoa hiyo walilazimika kuhamia kwenye maeneo mengine ya mikoa ya Shinyanga, Singida, Dodoma, Iringa, Mbeya hadi Rukwa kufuata malisho na maji. Uhamaji huo ulisababisha migongano kati ya wakulima na wafugaji, uharibifu wa mazingira na pia kuenea kwa ugonjwa wa sotoka katika maeneo yaliyohamiwa.

13. Mheshimiwa Spika, shughuli za uendelezaji wa ng’ombe wa maziwa ziliendelea vizuri na hasa kwa wafugaji wadogo wadogo nchini kwenye maeneo ambayo hayakukumbwa na ukame. Jumla ya mitamba 1,354 ilisambazwa kwa wafugaji ikilinganishwa na lengo la kusambaza mitamba 2,000. Sambamba na usambazaji wa mitamba, jumla ya mbuzi 200 wa maziwa walisambazwa kupitia shirika lisilo la kiserikali la “Heifer Project International”. Kutokana na sera kubadilika na Wizara kuacha kujishughulisha na biashara, mashamba ya Serikali ya kuzalisha mitamba

(LMUs) ya Sao Hill, Nkundi, Ibaga, Hanga, Lugufu, Mabuki, Kibaha, Mivumoni na Kahama yamepimwa ili kufahamu ukubwa na mipaka yake na pia kutambua mali zilizopo ili mashamba hayo yaweze kupatiwa hati miliki kwa madhumuni ya kubinafsishwa au kukabidhiwa taasisi zinazoweza kuendesha mashamba hayo kibiashara. Uongozi wa mikoa inayohusika utashirikishwa ili kuona kama wapo wawekezaji ndani ya mikoa wanaoweza kuendeleza shughuli hizo ili Serikali iendelee kutoa utaalamu wake.

14. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1996/97 shabaha kubwa ilikuwa ni kuongeza uzalishaji na ubora wa nyama, pamoja na kuendeleza masoko ya ndani na nje ili kuweza kulipatia taifa letu pato zaidi ikiwa ni pamoja na fedha za kigeni. Hata hivyo, hali ya uzalishaji nyama nchini iliendelea kukabiliwa na matatizo hasa kutokana na ukosefu wa maji na malisho katika sekta ya ufugaji wa asili kufuatia hali ya ukame iliyoikumba sehemu kubwa ya nchi yetu. Wizara imefanikiwa kupata fedha zilizotolewa na Serikali ya Japan jumla ya shilingi milioni 127 zitakazotumika kukarabati au kuimarisha malambo yaliyoathirika na ukame. Ugawaji na matumizi ya fedha hizi utategemea mapendekezo ya Wizara yangu yatakayopokelewa na viongozi wa Mikoa itakayohusika. Aidha Wizara inashauri wanavijiji kuendelea na juhudi za kuchanga fedha kwa ajili ya uchimbaji wa malambo.

15. Mheshimiwa Spika, ukame ulisababisha kutofikiwa lengo la uzalishaji wa nyama la tani 257,000 kwa msimu 1996/97. Kutokana na hali hiyo mifugo mingi ilikufa na wafugaji wengi walipata hasara kubwa kutokana na kuuza mifugo yao kwa bei ndogo ili kuepuka hasara. Kwa mfano Arusha bei ya ng'ombe mmoja ilishuka kutoka wastani wa shilingi laki moja hadi shilingi elfu tatu. Kwa niaba ya Serikali naomba nitumie nafasi hii kupitia kwa Waheshimiwa Wabunge kuwapa pole wafugaji wetu waliopatwa na baa hilo la kupotelewa na mifugo yao.

16. Kwa upande wa masoko ya mifugo ya ndani, Wizara iliendelea kukarabati vituo vya mifugo (night camps) katika mikoa ya Dar-es-Salaam, Tanga, Arusha, Tabora na Kilimanjaro. Lengo ni kukarabati minada ya mifugo na kuiweka katika mazingira mazuri ili ubinafsishaji wake uwe wa mafanikio. Katika mkoa wa Tanga kazi zifuatazo zimekamilishwa: njia za mifugo (stock routes), vituo 4 vya kulaza ng'ombe (night camps), kituo kimoja cha kukagulia mifugo (check point) kimejengwa na mnada wa ng'ombe unaendelea kujengwa Kibirashi (Tanga). Hivi sasa wafugaji wameanza kuvitumia vituo hivi. Minada ya mifugo ya Weruweru (Kilimanjaro), Themi na Makuyuni (Arusha) imepatiwa maji. Hata hivyo, suala la kuwa na machinjio mipakani ili kupunguza wimbi la mifugo yetu kuhama na kuchinjwa nchi jirani, pamoja na viwanda vya kusindika nyama vitapewa kipaumbele katika mwaka huu wa fedha, kwa kuwashirikisha wawekezaji.

17. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa vyakula vya mifugo nchini umekuwa wa wastani. Mashirika na makampuni ya watu binafsi, yana uwezo wa kuzalisha vyakula

mbalimbali vya mifugo na kufikia tani 381,000 kwa mwaka. Hata hivyo, viwanda vingi ama vimefungwa au vimekuwa vikizalisha chini ya uwezo wake kutokana na matatizo mbalimbali ikiwa ni pamoja na uchakavu wa mitambo, ukosefu wa malighafi, mtaji mdogo na mahitaji madogo ya vyakula hivi kutoka kwa wafugaji. Hii ni kutokana na wafugaji wengi kujitoa katika shughuli za ufugaji kunakosababishwa na biashara hizo kutolipa, bei ya mazao yao kuwa chini kulinganisha na bei kubwa ya vyakula hivyo, madawa na wakati mwingine kodi mbalimbali wanazotozwa wafugaji bila kuzingatia kipato chao. Katika kipindi cha mwaka 1996/97 tani 280,000 za vyakula mbalimbali zinakisiwa kuzalishwa.

18. Mheshimiwa Spika, nchi yetu inao uwezo wa kuzalisha ngozi milioni 3 kwa mwaka. Katika kipindi cha 1996/97 ngozi za ng'ombe milioni 1.5, mbuzi vipande milioni 1.0 na kondoo vipande 560,000 vilikusanywa ikilinganishwa na lengo la ukusanyaji ngozi za ng'ombe milioni 1.5, mbuzi vipande milioni 1.8 na kondoo vipande 800,000. Lengo la ukusanyaji halikuweza kufikiwa kutokana na kushuka kwa bei za ngozi nchi za nje. Kwa jumla uuzaji wa ngozi nchi za nje kwa mwaka 1996/97 ulikuwa ngozi za ng'ombe vipande 810,000, ngozi za mbuzi vipande 725,000 na ngozi za kondoo vipande 412,000 na kulipatia taifa shilingi 3,484 milioni.

**Huduma za Ushauri kwa Wakulima na Wafugaji**

19. Mheshimiwa Spika, Mradi wa Huduma za Ushauri kwa Wakulima na Wafugaji (NALERP) ulianzishwa mwaka 1989 na awamu ya kwanza ilikamilika rasmi mwezi Juni, 1996. Awamu ya pili (NAEP II) iliandaliwa na kuanza mwezi Oktoba, 1996 kwa madhumuni ya kuendeleza shughuli za ushauri zilizokuwa zinafanyika katika awamu ya kwanza pamoja na kujaribu kutatua matatizo ambayo hayakutatuliwa katika awamu hiyo. Maeneo muhimu yanayoshughulikiwa ni pamoja na kuwaelimisha wataalam na kuendelea kuwapatia nyumba na vitendea kazi, kuwapatia wakulima mafunzo ya kilimo na ufugaji bora, hifadhi ya ardhi na mazingira. Semina na mikutano mbalimbali kwa Viongozi wa wilaya katika mikoa yote 16 inayohusika isipokuwa mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma ilifanywa na imesaidia kuwafanya viongozi waelewe vizuri nini maana ya miradi hii. Maeneo mengine yanayohusika ni udhibiti wa magonjwa ya mifugo na mimea, malisho na afya ya mifugo. Mradi wa "Southern Highlands Extension and Rural Financial Services" unaosaidiwa na IFAD umeendelea kutekelezwa katika Mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini kwa kuwakopesha wakulima pembejeo na zana za kilimo. Miradi mingine inayotoa huduma za ushauri ni pamoja na mradi wa "Sasakawa Global 2000" na Mradi wa Kuendeleza Ng'ombe wa Maziwa.

**Upatikanaji wa Pembejeo**

20. Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza upatikanaji na usambazaji wa pembejeo Wizara yangu kwa kupitia katika Mfuko wa Pembejeo za kilimo na mifugo katika kipindi cha 1996/97 iliwakopesha mawakala wa pembejeo (stockists) jumla ya shilingi bilioni 1.7, zikiwa shilingi bilioni 1.1 kutoka HAZINA na shilingi milioni 600

kutokana na marejesho ya mikopo ya mwaka 1995/96. Aidha Wizara imeendelea kuwahimiza na kuwashirikisha kikamilifu wanunuzi wa mazao ya tumbaku, pamba na kahawa katika kuagiza na kusambaza pembejeo. Utaratibu huu pia umetumika kwa kuvihusisha Vyama vya Ushirika hususan pembejeo za zao la korosho katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Uchangiaji wa mifuko ya kuendeleza mazao umeendelea kwa nia ya kuboresha upatikanaji wa pembejeo, kuimarisha utafiti na huduma kwa wakulima ili kupunguza kero za wananchi. Nawapongeza wote waliochangia katika mifuko hiyo. Vile vile wakulima wameendelea kuhimizwa kujiunga na Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa (Savings and Credit Cooperative Societies) ili wanachama waweze kununua pembejeo wakati wanapohitaji kwa kutumia fedha zao bila kukopa kutoka Mashirika au Taasisi za fedha. Hata hivyo, matatizo makubwa yanayoukabili mfuko huu ni uhaba wa fedha ikilinganisha na mahitaji yake, wakati tunahitaji angalau kiasi cha shilingi 9 bilioni, lakini upatikanaji wake ni shilingi 1.1 bilioni. Mwaka jana, kati ya shilingi 3.5 bilioni zilizoidhinishwa na Bunge, fedha zilizopatikana kutoka Hazina na zile za marejesho zilikuwa jumla ya shilingi 1.7 bilioni tu.

21. Mheshimiwa Spika, kiasi cha tani 13,000 za aina mbali mbali za mbegu bora zilizalishwa katika msimu wa mwaka 1996/97. Lengo letu la tani 12,800 lilifikiwa kutokana na kuongezeka kwa wazalishaji ambao ni TANSEED, CARGIL, PANNAR, ALPHA SEEDS, INCOFIN TANZANIA LTD, ROTIAN, EAST AFRICAN SEEDS, CHRISTIAN COUNCIL OF TANZANIA, Mashamba ya mbegu ya Taifa na ya Mikoa, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na miradi mbalimbali iliyoshirikisha wakulima. Aina za mbegu bora zilizozalishwa na kusambazwa ni pamoja na mahindi ya chotara na ya mchanganyiko, mtama (Serena, Tegemeo na PATO), mpunga, ngano, maharage, ufuta, alizeti, soya, mboga na mbegu za malisho. Aidha wakulima walitumia mbegu zao walizohifadhi ambazo nyingi ni kutokana na vyanzo vya mbegu bora iliyozalishwa msimu wa 1995/96. Kutokana na ukame uliojitokeza na kutokuwa na mvua za kutosha katika Mikoa inayopata mvua za vuli, wakulima walilazimika kurudia kupanda mashamba yao hivyo kusababisha upungufu wa mbegu zinazokomaa mapema za mahindi, mtama na mikunde. Hata hivyo Serikali ilitoa kiasi cha tani 413 za mbegu kwa Mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Pwani na Lindi. Pia Serikali imetoa fedha kwa ununuzi wa mbegu za mihogo na viazi kwa Mikoa iliyotajwa ili kukabiliana na baa la njaa.

22. Mheshimiwa Spika, makadirio ya mahitaji ya mbolea kwa msimu wa 1996/97 yalikuwa tani 187,000 ya aina mbalimbali za mbolea ambayo ni asilimia 72 ya mahitaji ya msimu uliopita wa 1995/96. Hadi kufikia mwezi Mei, 1997 tani 150,000 sawa na asilimia 80.2 ya mahitaji zilikuwa zimewasili nchini na kusambazwa. Pamoja na kiasi kikubwa cha mbolea kusambazwa mikoani hali halisi inaonyesha kuwa kuna upungufu wa matumizi ya mbolea hizo kutokana na bei kuwa kubwa. Aidha mbolea hazikutumika kwa wingi kutokana na uhaba wa mvua za vuli na kuchelewa mvua za masika.

23. Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa madawa ya kilimo ulikuwa sio wa kuridhisha kutokana na kutoagizwa kwa wingi katika msimu uliopita. Kwa mazao ambayo yameingizwa katika soko huria kama kahawa, pamba, tumbaku, korosho wanunuzi wa mazao hayo wakiwemo makampuni makubwa na wafanyabiashara binafsi katika baadhi ya mikoa kama Mbeya, Kilimanjaro, Tabora, Mtwara, Lindi, Mwanza, Shinyanga na Arusha wamejiwekea utaratibu wa kusambaza madawa wao wenyewe. Kutokana na utaratibu huu mazao ya korosho na tumbaku hayakuwa na matatizo ya upatikanaji wa madawa na pembejeo nyingine kwa ujumla.

24. Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa zana za kilimo ulikuwa wa kuridhisha kutokana na kuwepo kwa wafanya biashara wengi wanaojihusisha na uagizaji wa zana hizi kwa wingi. Aidha kuanza tena kwa kiwanda cha UFI kutengeneza zana kutaziba pengo. Upungufu ulijitokeza katika upatikanaji wa majembe yanayokokotwa na wanyama yaani maksai kutokana na uagizaji pamoja na uzalishaji kuwa mdogo.

25. Mheshimiwa Spika, kwa ujumla upatikanaji wa madawa ya mifugo umekuwa wa kuridhisha kutokana na Sekta binafsi kushiriki katika ununuzi na usambazaji wa madawa hayo. Hata hivyo bei za madawa hayo zimeendelea kupanda na hasa kwa madawa ya majosho. Usambazaji wa madawa ya chanjo haukukidhi mahitaji kutokana na uhaba wa majokofu hasa kwenye maeneo ya wafugaji. Bado jitihada itabidi ziendelee kwa kuutaka uongozi wa Halmashauri zetu za wilaya zitenge baadhi ya fedha zinazotozwa kama ushuru wa mifugo zitumike katika kununulia dawa hasa ya uogeshaji mifugo pamoja na chanjo kwa mifugo.

**Mafunzo ya Wataalam, Wakulima na Wafugaji**

26. Mheshimiwa Spika, idadi ya wakulima na wafugaji 1640 walipata mafunzo katika fani mbalimbali za kilimo na mifugo kupitia vyuo vya Kilimo na Mifugo. Idadi hii ni ndogo ikilinganishwa na lengo la wakulima na wafugaji wapatao 4,000 waliotarajiwa kupata mafunzo. Sababu kubwa ya upungufu huu ni uhaba wa fedha. Aidha wataalam 142 walijiunga na mafunzo ya astashahada na stashahada na wote wanajigharamia, na wakati huo huo wanafunzi 102 walihitimu katika vyuo vyetu. Vile vile jumla ya wafanyakazi wapatao 660 walipata mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi. Sambamba na mafunzo haya, Wizara yangu ilitimiza ahadi yake ya kurekebisha mitaala (curricula) ya mafunzo ili kuwawezesha wanafunzi wa kujitegemea kuchukua mafunzo ya fani wanazopenda kwa muda mfupi wa kati ya miezi mitatu na sita. Muhtasari huu mpya utaanza kutumika katika mwaka mpya wa mafunzo unaoanza mwezi Septemba, 1997. Aidha kazi nyingine iliyotekelezwa ni pamoja na kutilia mkazo somo la biashara na menejimenti ya miradi midogo. Mitaala ya mafunzo kwa ajili ya wanafunzi na walimu imetayarishwa isipokuwa mafunzo hayakuanza kutokana na ukosefu wa fedha.

**Udhibiti wa Magonjwa, Wadudu na Ndege Waharibifu wa Mimea na Mifugo**

27. Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 1996/97 Wizara yangu iliendelea na jukumu la kudhibiti uharibifu wa mazao unaosababishwa na magonjwa, wadudu (dumuzi, nzige wekundu na viwavi jeshi) na wanyama waharibifu kama panya katika mashamba na maghala. Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Udhibiti wa Nzige Wekundu (IRLCO - CSA), Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO), Serikali ya Ubelgiji na Shirika la Misaada la Ujerumani (GTZ) iliangamiza jumla ya makundi 137 ya nzige wekundu. Aidha baadhi ya makundi ya nzige yalitoroka na kuvamia mashamba katika mikoa ya Kigoma, Rukwa, Tabora, Shinyanga na Mwanza. Udhibiti wa ndege waharibifu wa nafaka (Quelea quelea) ulifanyika katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Singida, Shinyanga na Tabora kwa kutumia ndege ya Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani (DLCO-EA) na hivyo kuokoa kiasi kikubwa cha mazao.

28. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1996/97 Wizara yangu ilipata taarifa ya ugonjwa wa mahindi katika wilaya za Mbinga na Songea. Baada ya kufanya uchunguzi, wataalamu wa kilimo wamegundua kuwa ugonjwa huu ni *"grey leaf - spot"* unaosababishwa na aina ya ukungu uitwao "*cercospora zea - maydis"*. Ugonjwa huu hushambulia zaidi majani ya mahindi na kuyafanya kuwa na mabaka yenye rangi ya kahawia. Mashambulizi yakizidi majani hupoteza rangi ya kijani kibichi na kuonekana yameungua au kukauka. Inakisiwa kuwa ugonjwa huu umeingizwa na mbegu zilizoagizwa kutoka nje ya nchi kati ya msimu wa 1994/95 na 1995/96. Kuna njia kuu mbili za kupunguza madhara ya ugonjwa huu. Ya kwanza ni kutumia mbegu zenye kustahimili ugonjwa na ya pili ni kutumia mbinu bora za kilimo. Mbegu aina ya H 614 na H 6302 zimeonyesha kustahimili ugonjwa huu, ingawa haieleweki uwezo huo utadumu kwa miaka mingapi. Aidha Wizara yangu itafanya utafiti kutafuta mbegu bora zaidi. Wakati utafiti unaendelea wakulima wanashauriwa kutuma mbegu aina H 614 na H 6302 pamoja na mbinu bora za kilimo. Wakati huo huo, Wizara itaandaa na kufanya utafiti wa kina kuhusu mdudu aitwaye "*Pink Bollworm*" anayesababisha kuwepo karantini ya kutozalisha zao la pamba katika mikoa ya Kusini ili tiba ipatikane kwa kushirikiana na majirani wa nchi ya Msumbiji.

29. Katika msimu wa 1996/97 mikoa ya kusini hasa Lindi ilikumbwa na baa la panya. Wizara yangu ikisaidiana na viongozi na wakulima wa Mkoa wa Lindi ilishiriki kikamilifu kwa kutoa wataalam, usafiri, chambo na sumu ya panya. Kampeni ya kuangamiza panya hao ilifanyika katika vijiji 132 kati ya vijiji 362 na kupunguza idadi ya panya kwa asilimia 70.

30. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1996/97 uzalishaji wa wadudu aina ya *"Neochetina sp."* uliendelezwa katika kituo cha Kibaha ili kuweza kupata wadudu ambao watapelekwa katika vituo vya uzalishaji vitakavyoanzishwa kwenye ukanda wa ziwa Victoria na baadaye kusambazwa ziwani kudhibiti gugu maji. Wataalam walifanya uchunguzi katika maeneo ya mto Pangani na mto Sigi ili kuona ni kwa

kiasi gani *"Neochetina sp."* wameweza kudhibiti magugu maji na pia kujua wameweza kuenea kwa kiasi gani. Matokeo katika sehemu walikosambazwa wadudu hao ni kwamba magugu maji yamenyauka na kufa. Hii inaonyesha jinsi wadudu hao wanavyoweza kudhibiti magugu hayo. Pia wadudu wameonekana kuenea katika maeneo mengine ya mito hiyo na hivyo kuendelea kudhibiti magugu maji. Ili tuweze kudhibiti gugu maji hili, ni lazima tukomeshe chanzo chake.

31. Mheshimiwa Spika, moja kati ya majukumu makubwa ya Wizara yangu ni kudhibiti magonjwa ya mifugo. Kati ya magonjwa yanayoathiri sana mifugo hapa nchini ni pamoja na sotoka, homa ya mapafu (CBPP), nagana na kichaa cha mbwa. Kutokana na taarifa iliyopatikana mwishoni mwa mwaka 1996 kuhusu kuwepo kwa mlipuko wa sotoka katika nchi jirani ya Kenya, Wizara yangu ilichukua hatua madhubuti ya kuchanja mifugo ili kuipa kinga dhidi ya ugonjwa huo hasa katika wilaya za Monduli, Arumeru, Hai, Karatu, Rombo na Ngorongoro ambapo ng'ombe 287,000 walichanjwa kati ya lengo la kuchanja ng'ombe 610,000. Pamoja na kazi ya uchanjaji kufanyika katika mazingira magumu ya uhaba mkubwa wa vifaa na dawa za kinga, kazi hiyo ilikuwa ya mafanikio kutokana na msaada kutoka Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU) na Shirika la Chakula la Umoja wa Mataifa. Chanjo za homa ya mapafu kwa ng'ombe zilifanyika katika mikoa ya Iringa, Morogoro, Rukwa, Tabora, Mara, Mbeya, Arusha, Kigoma, Kagera, Shinyanga na Singida. Lengo lilikuwa kuchanja jumla ya ng'ombe milioni 3. Hadi kufikia mwisho wa mwezi Mei 1997, jumla ya ng'ombe milioni 1.015 walikuwa wamepata chanjo ya kwanza.

32. Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa kichaa cha mbwa umekuwa ni tatizo kubwa kwa mikoa yote nchini. Jumla ya matukio 1200 ya watu kuumwa na mbwa na baadhi yao kufariki yalitolewa taarifa. Kwa kushirikiana na Wizara ya Afya juhudi mbalimbali zimefanywa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi juu ya athari ya ugonjwa huu na hatua za kuchukua mara mtu yeyote anapokuwa ameumwa na mbwa au mnyama pori. Aidha Wizara yangu ilitoa shilingi 20 milioni kwa ajili ya kununulia risasi na dawa ili kuua au kuchanja mbwa na paka katika maeneo ya matukio. Kazi hii inaendelea hadi hivi sasa.

**Umwagiliaji**

33. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa umwagiliaji Wizara yangu iliendelea kusimamia utekelezaji wa ujenzi na ukarabati wa miradi midogo midogo ya wakulima vijijini. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa na kufikia hatua mbalimbali kwa kushirikiana na Wafadhili ni kama:-

(1) Mradi wa kuendeleza mkulima mdogo katika mabonde ya mto Pangani na Rufiji/ Ruaha (River Basin Management and Smallholder Irrigation Improvement Project) umepata mkopo kutoka Benki ya Dunia. Chini ya mradi huu maeneo yanayofaa kuendelezwa yamekwisha tambuliwa, vifaa vimeandaliwa na uhamasishaji katika ngazi za wilaya umefanyika.

(2) Miradi ya Kitivo (hekta 640) na Mwamapuli (hekta 600) ambayo inapata mkopo

kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na inakaribia kukamilika. Utekelezaji wa miradi hii ulikuwa mdogo kutokana na kukosekana kwa fedha za hapa.

(3) Mradi wa Usangu unaopata msaada kutoka UNDP unategemea kuendeleza hekta 3,000 katika vijiji 6 vilivyoko katika bonde la Usangu. Mpaka sasa kiasi cha hekta 1,800 zimekwisha kamilika. Hata hivyo utekelezaji uliarithiwa na uhaba wa fedha za hapa.

(4) Mradi wa kukarabati kilimo cha umwagiliaji wa jadi katika Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha (hekta 4000). Mradi huu ambao unapata msaada kutoka UNDP umewezesha kukarabati sehemu muhimu za kutolea maji (weir and intake structures) katika vijiji vinne.

(5) Mradi wa "Smallholder Development Project for Marginal Areas" unaoendeleza mkulima mdogo katika mikoa mitano ya ukame (Tabora, Shinyanga, Dodoma, Mwanza na Singida) unaopata mkopo kutoka IFAD ulikamilisha ujenzi wa miradi midogo mitano yenye hekta zipatazo 1,300. Mradi unategemewa kukamilika na kukabidhiwa kwa wakulima mwaka 1997/98.

(6) Mradi wa Hombolo (Dodoma) unaopata msaada kutoka Serikali ya Italia uliendelea kukabiliwa na tatizo la ukosefu wa "drainage system" na udhaifu wa uongozi wa umoja wa wakulima. Mradi huu unategemea kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwenye eneo lenye jumla ya hekta 300.

(7) Mradi wa Madibira unapata mkopo kutoka ADB na una lengo la kuendeleza hekta 3000 mkoani Mbeya. Maandalizi ya awali ya kambi/nyumba, ajira ya wataalam na usanifu yamekamilika. Aidha maandalizi ya shughuli za kilimo yanaendelea katika eneo hilo.

**Utafiti wa Mazao ya Kilimo na Mifugo**

34. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utafiti, Wizara yangu iliendelea kutekeleza Programu ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo (National Agricultural and Livestock Research Program - NALRP). Katika kutekeleza shughuli za utafiti, mkazo umetiliwa zaidi katika kuyapa kipaumbele mazao ambayo yanaweza kufanyiwa utafiti kikanda (zonal priorities), kwa madhumuni ya kuwa na utafiti madhubuti wenye gharama ndogo ambao matokeo yake yanaweza kumsaidia mkulima katika kuongeza uzalishaji.

35. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1996/97, vituo vya utafiti vilifanikiwa kuzalisha mbegu bora mpya ya maharage iitwayo "Uyole 96" katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo huzaa mapema, huvumilia magonjwa pamoja na ukame. Wakulima wameshirikishwa katika uzalishaji na usambazaji wa aina hii ya mbegu ya maharage. Aidha vituo mbalimbali vilishiriki katika kutathmini ubora wa mbegu za mahindi zilizozalishwa na kampuni binafsi za mbegu.

36. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1996/97, mikakati ya kushirikisha sekta binafsi katika kusaidia kufanya utafiti wa mazao ya biashara ulitekelezwa kwa baadhi ya mazao. Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania (Tea Research Institute of

Tanzania - TRIT) imeshaanzishwa. Vile vile uchangiaji wa utafiti katika mazao ya pamba, kahawa, miwa pamoja na korosho umeanza kwa kiwango kilichokubalika kati ya Bodi zinazohusika na Wizara. Mazungumzo yanaendelea na wazalishaji wa tumbaku, mkonge, pareto na shayiri ili waweze kuchangia utafiti wa mazao haya. Kwa mantiki hiyo, Serikali itakuwa na uwezo wa kushiriki zaidi kufanya utafiti wa mazao ya chakula pamoja na mifugo ili kuhakikisha uzalishaji wa mazao ya chakula unaoongezeka kitaifa. Aidha uimarishaji wa uhusiano mzuri kati ya utafiti na ushauri wa kilimo bora kwa wakulima (research extension farmer linkage) uliendelezwa katika maeneo yote nchini pamoja na kuandaa mpango kamambe wa kushirikisha uongozi wote wa wilaya mbali mbali nchini. Hadi kufikia mwezi Mei, 1997, kiasi kifuatacho kimechangwa kwa ajili ya utafiti wa kuendeleza mazao yafuatayo: Chai shilingi 94.6 milioni, Pamba shilingi 92.0 milioni, Korosho shilingi 197.0 milioni, Kahawa shilingi 78.9 milioni, miwa shilingi 60.4 milioni na shayiri shilingi 9.6 milioni. Mazao mengine nayo yameandaliwa mkakati wa kuyachangia kwa madhumuni ya kujitegemea sisi wenyewe.

37. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo - mseto, Wizara yangu bado inaendelea kutilia mkazo katika kutafiti aina mbali mbali ya miti ili kupata miti yenye sifa ya kuhifadhi ardhi, uzalishaji wa malisho bora na urutubishaji wa ardhi. Wizara yangu, ikisaidiana na mradi wa SADC/ICRAF inaendeleza kutafiti miti mbali mbali iliyoletwa nchini kwa ajili ya kilimo-mseto kuona kama inafaa kwa kilimo hicho kwenye mazingira yetu. Aina ya miti jamii ya *Acacia leptocarpa*, *Acacia crossicarpa na Acacia julifera* ambayo kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita ilikuwa inajaribiwa katika mashamba ya wanavijiji wilayani Tabora, Urambo na Shinyanga na inatoa matokeo mazuri. Wakulima wengi wameelekea kuipenda na wameanza kuipanda miti hiyo katika mashamba yao kwa matumizi ya kuni kwa kukaushia tumbaku na kurutubisha ardhi.

38. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utafiti wa mifugo, mafanikio yanaendelea kuwa mazuri. Hadi sasa dawa za chanjo dhidi ya magonjwa ya kimeta (anthrax) na chambavu (black quarter) zimeendelea kutengenezwa na Taasisi ya Utafiti wa Maradhi ya Mifugo Temeke kwa kiasi cha kutosheleza mahitaji ya nchi nzima. Aidha napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa katika jitihada za kumpunguzia mfugaji gharama za chanjo hizo, utafiti wa dawa ya “Temeke Combined Blackquarter and Anthrax Vaccine - TECOBLAX” umekamilika na umethibitishwa kitaifa. Kazi ya kutokomeza ndorobo kisiwani Unguja iliendelea kwa kushirikiana na Shirika la Nuklia la Kimataifa na imeonyesha mafanikio kwa kuwa hapakutokea maambukizo mapya ya vijidudu (protozoal transmission) tangu Septemba, 1996. Katika juhudi za kupunguza vifo vya kuku vijijini vitokanavyo na ugonjwa wa kideri (New Castle Disease) Wizara ilifanya majaribio dhidi ya ugonjwa huo kwa kutumia chanjo aina ya V4 ya kideri isiyohitaji jokofu. Katika vijiji vya Nitekela na Mtopwa wilayani Mtwara dawa hiyo ilionekana kuleta kinga ya kutosha kwa asilimia kati ya 60 - 70.

**Maendeleo ya Ushirika**

39. Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya uchumi wa ushindani, hali ya Ushirika imeendelea kuwa mbaya. Vyama vingi vya Ushirika bado havijajizatiti kukabiliana na mazingira mapya ya ushindani. Ushirika bado una mitaji midogo, wanachama wachache, na havina sifa ya kukopa kutoka benki za biashara. Mara nyingi mitaji hiyo midogo imekuwa ikisambazwa katika shughuli nyingi za hasara. Aidha udhaifu katika uongozi na menejimenti umeongeza kudidimiza miliki ya soko la ushirika baada ya soko huria kupamba moto. Baadhi ya vyama vimeshindwa kufanya biashara na kuashiria mwelekeo wa kufutwa.

40. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1996/97 idadi ya Vyama vya Ushirika vya Misingi vya Kilimo na Mifugo Vijijini vimepungua na kufikia 2,472 kutoka 2,525 vya mwaka uliopita. Hata hivyo idadi ya wanachama iliongezeka kidogo kutoka 317,053 hadi 362,584. Kwa hiyo idadi ya wakulima/wafugaji wanachama wa Vyama vya Ushirika ni asilimia 10 ya wakulima wote nchini. **Bado juhudi zinatakiwa kuwahamasisha wakulima na wafugaji waweze kujiunga na Ushirika ili waweze kuongeza nguvu na kuweza kupambana na ushindani katika mfumo wa soko huru.**

41. Mheshimiwa Spika, Vyama vingi vya Ushirika vya mazao mbali mbali kama kahawa, pamba, tumbaku na korosho viliendelea kupoteza sehemu kubwa ya soko na kulazimika kuwa wakala wa wanunuzi binafsi hivyo kupoteza sehemu kubwa ya ziada ambayo ingeweza kuwarudia wakulima. Pamoja na matatizo yaliyovikabili Vyama vingi vya Ushirika, vyama vya KCU na BCU viliweza kuhimili vema soko huru kwa kutumia mifuko yao ya kununulia mazao. Aidha kwa njia ya ubia Vyama vya Ushirika viliendelea kufanya biashara na Vyama vya Msingi.

42. Mheshimiwa Spika, Vyama vya Akiba na Mikopo vimeonyesha kukidhi kanuni za ushirika na msingi wa kujitegemea. Kuna vyama 906 kati ya hivyo vyama 440 ni vya wafanyakazi mijini na 466 ni vya wakulima na wafugaji vijijini. Hadi Desemba, 1996 amana katika Vyama vya Akiba na Mikopo zilifikia shilingi 1,997,403,514 na wanachama wa mijini walipata mikopo ya kiasi cha shilingi 759,212,265 na wa vijijini kiasi cha shilingi 276,043,832 ambayo kiasi kikubwa kimetolewa kwa Vyama vya Msingi vya mazao kwa ajili ya pembejeo na pia ununuzi wa mazao. Aidha wanachama walipata mikopo kwa ajili ya elimu, ujenzi wa nyumba na maendeleo mengine. Napenda pia kuwafahamishaWaheshimiwa Wabunge kuwa Benki ya Ushirika ya Mkoa wa Kilimanjaro ilifunguliwa rasmi tarehe 9 Agosti, 1996 na imeendelea vizuri kwa kuongeza amana kutoka shilingi milioni 26 hadi milioni 670 mwishoni mwa mwezi Machi, 1997.

43. Mheshimiwa Spika, Ushirika wa mifugo unayo nafasi kubwa ya kuleta maendeleo kwa wakulima na wafugaji. Kwa mfano, Chama Kikuu cha Wafugaji wa ng’ombe wa maziwa Tanga (Tanga Dairy Co-operative Union - TDC) kimekuwa na

maendeleo ya kuridhisha katika kipindi cha mwaka 1996/97. Ushirika wa aina nyingine kama wa viwanda na uvuvi umekuwa na maendeleo yasiyoridhisha kutokana na ukosefu wa mitaji. Aidha, Vyama vya Ushirika wa ujenzi wa nyumba vimesimamisha shughuli zake kutokana na ukosefu wa fedha na mapambano ya soko huru. Kazi ya ukaguzi na usimamizi, elimu na mafunzo kimsingi zimeathirika kutokana na upungufu wa watumishi na ukosefu wa nyenzo za kazi. Hadi mwezi Machi, 1997 Vyama vya Misingi 80 kati ya 4,917 na Vyama Vikuu 10 kati ya 44 vilikuwa vimekaguliwa mahesabu ya mwaka 1995/96. Takwimu hizi zinaonyesha dhahiri kuwa hali ya Ushirika siyo nzuri. Kumekuwepo na ubadhilifu katika Vyama vya Ushirika na Serikali imelazimika kuunda Tume za Uchunguzi mwaka 1996/97 ili kuvichunguza Vyama Vikuu vya KCU, BCU, KDCU, SAMCU, TAMCU, MBICU, MBOCU, KNCU na WETCU.

44. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ushirika Moshi kimeendelea kutoa mafunzo ya diploma kwa wanafunzi 230 na kozi fupi kwa washiriki 140, washiriki wa vikundi vya wanawake 3,000, watumishi wa Halmashauri 1,500 na makatibu wa vyama vya msingi 800 chini ya mfumo mpya wa kuchangia gharama za mafunzo. Hata hivyo vyama vingi vinashindwa kuwasomesha watumishi wao kwa kutotenga fedha za kutosha kwa ajili hii. Vile vile, Chuo cha Ushirika Moshi kina matawi kumi na mawili nchini. Kazi kuu za matawi haya ni kutoa elimu na mafunzo ya ushirika kwa vikundi, vyama mbali mbali (associations) kama vya wakulima na wafugaji na Vyama vya Ushirika. Elimu na mafunzo hayo huimarishwa pia kwa njia ya redio na masomo kwa njia ya posta katika fani mbali mbali za ushirika hasa mazao, akiba na mikopo, ujenzi wa nyumba, ufugaji na maduka.

**Soko Huru**

45. Mheshimiwa Spika, mwaka 1996/97 ni mwaka wa tatu tangu utekelezaji wa sera hii ya soko huru kwa mazao ya biashara uanze kutumika. Kwa muda wote huo, Wizara yangu imeendelea na kazi yake ya kuratibu, kushauri na kutoa miongozo na mazingira yanayofaa ili kufikia azma ya sera hii ambayo ni kuongeza ushindani wa kibiashara kati ya wafanyabiashara kwa manufaa ya wakulima wa mazao yanayohusika.

46. Mheshimiwa Spika, sera hii imeleta mafanikio ya kutoa changamoto katika sekta ya kilimo ya mazao ya pamba, korosho, tumbaku na kahawa. Baadhi ya mafanikio kama nilivyoelezea katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka uliopita wa 1996/97 ilikuwa ni pamoja na:-

(a) wanunuzi wameongezeka na kuimarisha ushindani
(b) bei kwa wakulima zimeongezeka kufuatia ushindani
(c) mara nyingi wakulima wamelipwa papo kwa papo, au baada ya muda mfupi
(d) uwezo wa Viwanda vya kuchambulia pamba na kukoboa kahawa umeongezeka,
(e) bei ya mkulima, mnunuzi wa mazao, na uuzaji nje imeweza kubainika mapema baada ya Wizara kuimarisha upatikanaji wa takwimu

47. Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo mafanikio, matatizo mbalimbali yamejitokeza yakiwemo ukiukaji kanuni na taratibu za ununuzi wa mazao kutozingatia ubora wa mazao na vipimo, ukwepaji wa malipo ya ushuru, wakulima kukopwa mazao yao ama kuwalipa bei ndogo ambazo hazizingatii gharama za uzalishaji. Wizara yangu inafanya mawasiliano ya karibu baina ya Bodi za mazao pamoja na wafanyabiashara ili kufanikisha utekelezaji wa soko huru. Ili kuondokana na tatizo la soko la mazao ambalo bado linatawaliwa na Bodi za Mazao, Wizara yangu imeandaa mkakati ambao utaruhusu mazao ya pareto, chai na mkonge yauzwe katika mfumo wa soko huru kuanzia msimu wa 1997/98 na kuendelea kadri maandalizi yatakavyokuwa yanakamilika.

**Marekebisho ya Muundo wa Wizara na Mashirika ya Umma**

48. Mheshimiwa Spika, chini ya mpango huu, Wizara yangu imeendelea kutekeleza sera ya Serikali ya kujiondoa katika shughuli za uzalishaji na za kibiashara kwa lengo la kuimarisha uwezo wake katika kutoa huduma muhimu kwa wakulima na wafugaji. Sambamba na utaratibu huu, Wizara imeanza kuwahamasisha washiriki (stakeholders) katika sekta kuunda vikundi mbalimbali (associations/councils, steering committees) kulingana na mazao au shughuli inayowahusu ili waweze kuwa na umoja (forum) na mahali pa kuzungumzia na kupanga mikakati ya pamoja ya kuendeleza zao au shughuli nyingine za mifugo inayowahusu. Hii ikiwa ni pamoja na kuanzisha mifuko maalum ya kuendesha shughuli muhimu kama vile utafiti, huduma za kitaalam, na pembejeo. Aidha, Wizara yangu inaendelea kuimarisha shughuli za utafiti ushauri kwa wakulima, kutoa taarifa za masoko, kukuza ushirika na vyombo vingine vya kumwendeleza mkulima kusimamia sera na sheria za kilimo, mifugo na ushirika.

49. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha utendaji, Wizara yangu inakamilisha muundo wa Wizara kuwezesha shughuli zake zifanyike kwa ufanisi zaidi. Kwa kipindi kirefu kumekuwa na mawasiliano na vyombo mbali mbali jinsi ya kuimarisha idara za Wizara hii kwa nia ya kuimarisha utendaji wa kazi. Ninafurahi kuliambia Bunge lako Tukufu kuwa kuanzia mwaka huu wa fedha, muundo huu utazingatia majukumu makuu (core functions) ya Wizara katika sekta za Kilimo, Mifugo, Utafiti na Maendeleo ya Ushirika. Aidha sekta ya Mifugo imepewa kipaumbele katika muundo huu ili kuweza kutekeleza kikamilifu masuala yote yanayohusu sekta hii, pamoja na maombi yenu Waheshimiwa Wabunge ambayo mlikuwa mnayasisitiza kila bajeti kuhusiana na umuhimu wa kuipa sekta ya mifugo nafasi yake.

50. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza muundo huu mpya Wizara imechuja viwango vya wafanyakazi katika kila sehemu ili kukidhi mahitaji halisi. Katika kufanya zoezi hili, imebidi kuhamisha au kupunguza wafanyakazi kufuatana na mahitaji halisi. Nia yetu ni kubaki na wafanyakazi 13,500 badala ya 19,522 waliokuwepo kabla ya kufanya zoezi la kupunguza wafanyakazi 6024 katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Kazi hii sote tunaelewa imekuwa ngumu na nzito

kutekelezwa kwa muda wa mwaka mmoja. Hata hivyo katika kipindi hiki, tutaendelea kuimarisha utendaji ili pale penye kasoro tupasawazishe na kupunguza kero kwa watumishi.

51. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika kipindi cha 1996/97 imeendelea kushirikiana na Tume ya Rais ya kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) katika kufanikisha urekebishaji na ubinafsishaji wa mashirika yaliyo chini ya Wizara. Taratibu za ubinafsishaji wa mashirika ambazo karibu zinakamilika ni za Mamlaka ya Mkonge (TSA), Bodi ya Pareto (TPB), Bodi ya Tumbaku (TTPMC) na Kampuni ya Viwanda vya Maziwa (TDL). Mashirika mengine yako katika hatua mbali mbali za uchunguzi na mazungumzo na wawekezaji ili hapo baadaye yaweze kubinafsishwa. Mashirika hayo ni kama Shirika la Taifa la Usagishaji (NMC), Kampuni ya Uendelezaji wa Ng'ombe wa Maziwa (DAFCO), Shirika la Taifa la Chakula na Kilimo (NAFCO), Shirika la Sukari (SUDECO), Mamlaka ya Chai (TTA), Kampuni ya Kuzalisha Mbegu (TANSEED) na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO). Kampuni ya Kusindika Nyama (TPL) ambayo ilikuwa kwa mfilisi (LART) hivi sasa imehamishiwa Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma ili iweze kufanyiwa utaratibu wa kubinafsishwa. Lengo la Serikali ni kumtafuta mbia ambaye ataendeleza shughuli za kusindika nyama, na mifugo kwa ujumla. Aidha uamuzi wa Serikali ni kuifilisi Kampuni ya KOTACO baada ya Wakorea waliokuwa na ubia na Serikali kujitoa.

52. Mheshimiwa Spika, zoezi la ubinafsishaji ambalo linaendelea hivi sasa linawagusa pia wakulima wadogo wadogo hasa katika Mashirika na Mashamba kama Bodi ya Pareto (TPB), Bodi yaTumbaku (TTPMC), SUDECO na Tanzania Dairies Limited (TDL). Kwa mfano kuhusu shamba la mifugo la Utegi, Wizara imekubaliana na PSRC kimsingi kuwa wapendekeze utaratibu wa kununua hisa katika shamba hilo kwa wananchi ambao maskani yao yapo karibu na shamba hilo. Aidha wakulima wadogo wadogo (outgrowers) wa mashamba ya miwa ya Mtibwa na Kilombero wameomba kupewa asilimia 15-20 ya jumla ya hisa ya Kampuni hizo. Wakulima hao wameunda chama chao na tayari wamechanga kiasi cha shilingi, 650 milioni za kununulia hisa ili kufaidika na ubinafishaji wa viwanda. Ombi hili litazingatiwa wakati wa kubinafsisha viwanda vya sukari. Pia wawekezaji katika Bodi za Pareto, Tumbaku na viwanda vya maziwa Tanga, Dar es Salaam na Arusha wamekubali kutenga hisa asilimia 10 mpaka 15 **bila malipo kutoka kwa wakulima,** na hivyo kuwezesha wakulima kupata kauli na faida bila kuchangia hisa moja kwa moja. Wizara itazidi kusisitiza utaratibu huu pale ambapo itadhihirika kwamba wakulima hawawezi kuchangia hisa moja kwa moja lakini wafaidike pale wanapotoa mazao yao katika viwanda vilivyo binafsishwa.

**Maendeleo ya Watumishi**

53. Mheshimiwa Spika, kati ya Wizara ambazo kwa muda mrefu zimekuwa na matatizo mengi ya watumishi ni pamoja na Wizara yangu hii. Sote tunaelewa matatizo

ambayo yamekuwa yakiwakabili watumishi wa Wizara hii. Wengi wao wamekuwa wakikaa kwenye cheo kimoja au ngazi moja ya mshahara kwa kipindi kirefu sana. Wapo watumishi waliokaa zaidi ya miaka 10 ambao kwa bahati mbaya hawajathibitishwa kazini au kupandishwa vyeo. Baya zaidi hata mishahara ya baadhi yao ilikuwa haijawahi kurekebishwa kwa kipindi chote hicho. Kazi iliyofanyika katika kipindi chote cha mwaka uliopita ilikuwa ni kuanza kuweka kumbukumbu sahihi za kila mtumishi na kuanzisha utaratibu wa kuwa na orodha ya mpangilio kwa kila mtumishi kufuatana na muda wake kazini, cheo alichonacho kama kinalingana na kanuni za utumishi na pia kuwapanga kufuatana na vigezo muhimu vya kanuni zinazotawala ajira ya kila mmoja wao. Hadi kufikia mwezi Mei, 1997 tulikuwa na watumishi 14,897 wa Wizara nzima. Kati ya hawa kuna Wakaguzi wa Vyama vya Ushirika 479 ambao watajiunga na Wizara kuanzia kipindi cha 1997/98. Tulikuwa na watumishi 373 ambao mishahara yao ilikuwa inalipwa nje ya kompyuta. Kati ya hao watumishi 276 mishahara yao imeingizwa kwenye kompyta mwezi Mei, 1997. Kwa watumishi waliosalia 97 uhakiki wa ajira zao umekamilika na tunatarajia mishahara yao kuingizwa kwenye kompyuta kuanzia mwezi huu Julai, 1997. Tumegundua pia kuwa kumekuwepo na udanganyifu wakati wa upunguzaji watumishi. Wengine wamehamishiwa Wizara nyingine kwa kukiuka taratibu zilizowekwa.

54. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1996/97 jumla ya watumishi 1977 walipandishwa vyeo. Aidha katika kipindi hiki watumishi 246 walithibitishwa kazini na 76 walipewa ajira za kudumu. Vile vile watumishi wa Uyole wapatao 429 walipewa barua rasmi za kuwarejeshwa Serikalini.

55. Mheshimiwa Spika, Wizara inasimamia kada 65 za taaluma mbali mbali zikiwa na ngazi 517 za mishahara. Zoezi la kupitia tange za kada na kurekebisha kasoro zilizokuwepo limekamilika. Baadhi ya wale waliopandishwa vyeo wamesereka kutokana na yaliyojitokeza baada ya marekebisho ya tange.

**Matumizi ya Fedha za Mpango wa mwaka 1996/97**

56. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 1996/97 Wizara pamoja na Mashirika yake ilitengewa jumla ya shilingi milioni 14,527.3 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi milioni 3,427.9 kwa ajili ya matumizi ya shughuli za maendeleo. Fedha za hapa zilikuwa shilingi milioni 1,022.9 na fedha za nje shilingi milioni 2,405.0. Kwa ujumla utekelezaji wa miradi haukuwa wa kuridhisha kufuatana na uhaba wa fedha. Hadi kufikia mwezi Mei, 1997 matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi milioni 8,712.8 sawa na asilimia 59.9 wakati matumizi ya fedha za mpango wa maendeleo yalikuwa shilingi milioni 105.0 sawa na asilimia 3.1.

## III MPANGOWA MAENDELEO WA MWAKA 1997/98

57. Mheshimiwa Spika, maelezo niliyotoa kwenye utekelezaji wa mpango wa mwaka jana yamedhihirisha upungufu mkubwa wa fedha za maendeleo uliyojitokeza. Hivyo kulazimu shughuli nyingi kuingizwa kwenye Mpango wa Mwaka 1997/98. Baada ya kuainisha majukumu makubwa na muundo mpya wa Wizara, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 1997/98 umeandaliwa kwa kuzingatia Sera za kijumla za kitaifa, Mwongozo uliotolewa na Tume ya Mipango pamoja na Hazina kuhusu utayarishaji wa Mpango wa Tano unaoendelea na Bajeti ya Upeo wa 1997/98 - 1999/2000, sera za Kilimo na Mifugo pamoja na Ushirika na muundo mpya wa Wizara. Mpango wa Maendeleo wa mwaka 1997/98 unalenga katika kuimarisha na kuboresha majukumu muhimu ya Wizara ya Kilimo na Ushirika.

**Huduma za Ushauri kwa Wakulima na Wafugaji**

58. Mheshimiwa Spika, huduma za ushauri kwa wakulima na wafugaji zitaendelea kuimarishwa kwa kutekeleza miradi ya “National Agricultural Extension Project (NAEP II)”, “Southern Highlands Extension and Rural Financial Services (SHERFS)”, “Sasakawa Global 2000” na miradi ya Uendelezaji wa Ng’ombe wa Maziwa inayotoa huduma hizo. Aidha Wizara itaendelea kushirikiana na mashirika yanayosaidia miradi hii yakiwemo Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Jumuia ya Ulaya (EU), IFAD, WFP, Serikali za Uholanzi na Uswisi. Miradi hii itaendelea kuimarisha huduma za ushauri kwa kuwapatia wataalam vitendea kazi, kujenga nyumba za wataalam vijijini, pamoja na kutoa mafunzo kwa wataalam na wakulima kuhusu kilimo na ufugaji bora, hifadhi ya ardhi na mazingira.

**Uzalishaji Mbegu Bora**

59. Mheshimiwa Spika, kutokana na sera ya Serikali ya kutojihusisha na shughuli za kibiashara, kazi ya kuzalisha mbegu za kizazi kilichothibitishwa (certified seeds) itaendelea kufanywa na Makampuni binafsi, Mashirika yasiyo ya Ki-Serikali na taasisi nyingine mbalimbali. Wizara yangu, itaendelea kutafiti, kutunza vizazi vya mbegu (Parental Material), kukuza vizazi vya awali (Breeder Seeds) na vya msingi (Foundation Seeds) ili kudhibiti Haki Miliki (Breeders Rights) ya mbegu zilizotolewa na Serikali.

60. Mheshimiwa Spika, ili kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mbegu, mikakati ifuatayo itatekelezwa katika kipindi cha 1997/98:-

(a) kwa kusaidiana na Serikali ya Denmark, Wizara itaanzisha uzalishaji wa mbegu kwa kutumia wakulima wadogo wadogo, vikundi vya akina mama na ushirika. Mpango huu utahusu mazao muhimu ya chakula na ambayo kampuni za mbegu hazijihusishi. Utaratibu huu utawawezesha wakulima kupata mbegu bora kwa bei nafuu zaidi.

(b) Taratibu za kurekebisha na kubinafsisha Kampuni ya Taifa ya Mbegu (TANSEED) zinakamilishwa ili kampuni iwe na uwezo mkubwa wa kuzalisha na kusambaza mbegu nchini. Aidha Wizara yangu itaendelea kuhamasisha sekta binafsi ili ishiriki kikamilifu kwenye uzalishaji wa mbegu.

(c) Wizara inakamilisha taratibu za kutunga sheria ya Hati Miliki (Plant Breeders Rights Legislation) kwa aina zote za mbegu zitakazotolewa kisheria na Kamati inayosimamia mbegu bora nchini. Sheria hii italinda na kuhakikisha matumizi halali ya mbegu zote zinazotolewa na Serikali na sekta binafsi.

**Uzalishaji wa Mboga, Matunda na Viungo**

61. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka mingi iliyopita mazao haya hayakupewa kipaumbele katika nyanja za utafiti na uzalishaji. Hata yale yanayozalishwa hayakidhi sifa za wanunuzi wa nje ya nchi au hukosa soko kutokana na uhaba wa viwanda vya kusindika au vyombo vya kuhifadhi. Kwa kuzingatia umuhimu wa mazao haya Wizara itaendelea kuimarisha kituo cha utafiti wa uzalishaji wa mbegu za mboga na matunda kilichopo Tengeru, Arusha. Aidha kuna mipango ya kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje ili kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika matunda. Kwa upande wa viungo vya chakula kama iliki, pilipili manga na mdalasini Wizara yangu itaendelea kutoa msukumo wa kuzalisha mazao haya ambayo yameonyesha kuwa na soko la ndani na nje ya nchi.

**Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo na Mifugo**

62. Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo na mifugo, Wizara itaendelea kuweka mazingira mazuri ili sekta binafsi iweze kushiriki kikamilifu katika uagizaji na usambazaji wa pembejeo. Katika msimu wa 1997/98 Wizara itashughulikia suala la pembejeo kama ifuatavyo:-

(a) kuendeleza Mfuko wa Pembejeo za kilimo na mifugo.

(b) kuhamasisha na kuhimiza wanunuzi wa mazao ya kilimo na mifugo washiriki pia katika kuagiza na kusambaza pembejeo,

(c) kuchangia mfuko wa kuendeleza mazao katika utafiti na huduma kwa wakulima.

(d) kuwahimiza wakulima wajiunge na Vyama vya Kuweka na Kukopa (Savings and Credit Societies) ili kurahisisha upatikanaji wa fedha (mikopo) kwa ajili ya kununulia pembejeo.

(e) kuendelea kuhimiza Halmashauri zenye mifugo mingi zianzishe utaratibu wa kuweka mapato yatokanayo na ushuru wa mifugo ili yatumike katika kununulia madawa na kuboresha huduma za majosho.

**Umwagiliaji**

63. Mheshimiwa Spika, kama tunavyoelewa kwa muda mrefu kilimo chetu kimeendelea kutegemea mvua hali ambayo husababisha kutokuwa na uhakika wa uzalishaji hasa nyakati za ukame. Kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu mwaka jana, Wizara yangu ilikwishatayarisha mpango wa muda mrefu wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji unaosisitiza uendelezaji wa kilimo hicho kwa wakulima wadogo wadogo, kwa kuvuna maji katika maeneo yenye ukame na kuwawezesha wakulima kuanzisha umoja wao wa umwagiliaji. Katika mpango huu, uendelezaji wa mabonde umepewa kipaumbele pamoja na kuhifadhi mazingira katika vyanzo vya maji na

maeneo yanayohusu umwagiliaji. Kwa matinki hiyo Wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Maji imeanza kwa kutekeleza mradi wa kuendeleza wakulima wadogo katika mabonde ya mito ya Pangani na Rufiji. Maeneo yanayohusika katika bonde la mto Pangani ni Lekitatu (Arumeru) na Mombo (Korogwe). Kwa upande wa bonde la mto Rufiji ni Ipatagwa (Mbarali) na Luganga (Iringa Vijijini). Maeneo haya yote yamekwisha kufanyiwa savei na usanifu. Ujenzi wa mifereji utaanza mwaka huu.

64. Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo, kazi kubwa tutakayoifanya katika kipindi cha 1997/98 ni kushirikiana kwa karibu zaidi na Wizara ya MAJI ili mpango wowote uwe na uwiano na Wizara hiyo. Aidha Wizara itaendelea kufuata utaratibu wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa kulenga mabonde ya mito badala ya kufuata mipaka ya kiutawala. Wizara yangu pia itashughulikia kilimo hiki kwa kutoa kipaumbele kwa kuendeleza mashamba ambayo wakulima wadogo wanaweza kumudu kuyaendesha kuliko kuanzisha miradi mikubwa ambayo imekuwa ni mzigo kwa Taifa na wakulima wadogo. Hata hivyo katika kipindi hiki Wizara itatekeleza shughuli zifuatazo:

(a) kuhamasisha na kushauri sekta ya watu binafsi ya wakulima wadogo wadogo na wakubwa katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji,

(b) kuhamasisha uanzishaji na uimarishaji wa ushirika wa wakulima wamwagiliaji (Water Users Association/Water Users Cooperative Societies),

(c) kuanza rasmi utekelezaji wa mradi wa kitaifa unaohusisha uendelezaji wa umwagiliaji kwa wakulima wadogo wadogo chini ya “Tanzania Agricultural Sector Programme Support” kwa msaada wa fedha kutoka DANIDA. Mradi huu utatekelezwa katika maeneo ya wilaya ya Iringa vijijini (1997/98), wilaya za Morogoro vijijini na Iringa vijijini (1998/99) na wilaya za Mbeya vijijini, Morogoro vijijini na pia Iringa vijijini (1999/2000). Wilaya nyingine zitaendelea kufanyiwa utafiti na upembuzi yakinifu ili nazo ziingie kwenye mpango kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana. Hata hivyo tutaendelea kuwahamasisha wakulima wengine waendelee na kilimo hiki bila kusubiri kuwekwa kwenye mpango maalum.

**Utafiti wa Mazao na Mifugo**

65. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itashirikiana na Benki ya Dunia na wafadhili wengine kutekeleza utafiti wa kilimo na mifugo chini ya mradi wa kitaifa wa “Tanzania Agricultural Research Project (TARP II)”. Katika kipindi cha 1997/98 utafiti utamlenga mkulima zaidi katika kutatua matatizo yake na siyo anayotaka mtafiti. Utafiti wa mazao na mifugo kwa 1997/98 utaweka mkazo wa pekee katika shughuli za utafiti wa mazao ya chakula na biashara na usambazaji wa matokeo yake kama ifuatavyo:-

(a) Kutafiti aina bora za mbegu za mazao ya chakula na biashara zenye kutoa mavuno mengi, kuhimili magonjwa na ukame.

(b) Kubuni na kupendekeza mbinu bora za kilimo cha mazao. Mkazo utawekwa katika kushirikiana na mtandao wa utafiti wa mazao yaliyoko katika kanda zinazohusika.

(c) Kutafiti mbinu bora na za gharama nafuu za kudhibiti wadudu waharibifu, magonjwa na magugu sugu ya mazao ya chakula na biashara.

(d) Kuimarisha uwiano baina ya utafiti, ushauri kwa wakulima na wakulima wenyewe (research extension farmer linkage) kwa lengo la kuboresha kilimo na ufugaji.

(e) Mkazo utatiliwa zaidi katika utafiti kwenye mashamba ya wakulima (on-farm research) kwa kuwahusisha wakulima wenyewe kutoka mwanzo wa utayarishaji wa majaribio hadi mwisho wa majaribio hayo.

(g) Kutafiti na kutathmini vifaa vya hifadhi ya chakula, zana za kukokotwa na ng'ombe na usafirishaji mazao kwa kutumia wanyama kazi (draught animals),

(h) kuendeleza jitihada za utambuzi wa ugonjwa wa Homa ya Mapafu hapa nchini kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO),

(i) kuendeleza kuchunguza viwango vya Samorin kwenye damu ya ng'ombe (antigen/ELISA) kwa madhumuni ya kujua kiwango kinachotosha kutibu ugonjwa wa ndorobo.

**Udhibiti wa Magonjwa, Wanyama na Wadudu Waharibifu wa Mimea na Mifugo**

66. Mheshimiwa Spika, hali ya milipuko ya nzige inaelekea kuendelea pia mwaka huu kwa sababu ya makundi ya nzige yaliyoanza kuonekana katika mbuga za Bahi, Iku, Malagarasi na Wembere. Wizara yangu imeanza kujiandaa kupata nyenzo na dawa za kutosha kukabiliana na milipuko hiyo. Aidha maandalizi yanaendelea ya udhibiti wa 'quelea quelea' mara watokeapo. Wizara yangu kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika itatekeleza mradi wa Hifadhi Mazingira Ziwa Victoria unaoshughulikia udhibiti wa magugu maji, na hifadhi ya ardhi kando kando ya Ziwa hilo. Taasisi, Jumuia na wananchi walioko kando kando ya Ziwa Victoria wataendelea kuhamasishwa ili washiriki katika udhibiti wa magugu maji.

67. Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti ugonjwa wa mihogo, malengo ya mwaka 1997/98 ni pamoja na kuzalisha kwa wingi wadudu maadui wa kidung'ata watakaosambazwa katika mikoa ya Mwanza, Mtwara, Lindi na Morogoro. Aidha huduma za karantini za kudhibiti uingizaji na usafirishaji wa mimea nchini zitaimarishwa katika vituo vilivyoteuliwa kulingana na sheria mpya ya Hifadhi ya Mimea na Kinga ya Mazao. Vituo hivyo ni: viwanja vya ndege vya Kimataifa vya Dar-es-Salaam na Kilimanjaro, bandari za Tanga, Dar-es-Salaam, Mtwara na bandari zilizopo katika maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa na pia vituo vilivyopo katika mipaka ya nchi yetu. Kampeni ya kudhibiti panya itaendelezwa katika awamu ya pili kwenye vijiji 230 vilivyosalia kati ya vijiji 362 katika mkoa wa Lindi ili kupunguza uharibifu wa mazao.

68. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo mradi mpya wa ujirani mwema wa kudhibiti ndorobo Afrika Mashariki unatarajiwa kuanzishwa katika maeneo ya mipakani kwa kushirikiana na Serikali ya Uganda na Kenya kwa msaada kutoka

Jumuia ya Nchi za Ulaya (EU). Wizara yangu itaendelea na juhudi za kupambana na sotoka na homa ya mapafu. Aidha uchanjaji wa ng'ombe dhidi ya kupe na ndigana kali kwa ng'ombe wa maziwa utaendelea. Ili kukabiliana na ugonjwa wa kichaa cha mbwa Wizara yangu itashirikiana na Wizara za Maliasili na Utalii, na Wizara ya Afya kuendesha kampeni ya kuchanja mbwa na paka na kuua wale wanaozurura ovyo mitaani pamoja na kuelimisha wananchi kuhusu athari za kichaa cha mbwa.

**Mafunzo**

69. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1997/98 Wizara yangu itaendelea kutilia mkazo mafunzo ya wakulima na wataalam kwa lengo la kuwapatia mbinu na teknolojia mpya kulingana na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia. Pia mafunzo yatalenga katika kuwawezesha wahitimu kujiajiri wenyewe. Kozi fupi za namna hiyo zinaweza kuandaliwa hata kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanaoshughulikia kilimo au ufugaji. Aidha mpango wa kuchangia gharama za mafunzo utaendelea. Kwa mwaka huu wa fedha wa 1997/98 Wizara ina mpango wa kuwapatia masomo watumishi 110, wanafunzi tarajali 70 ambao watachangia asilimia 40 ya gharama za chakula kwa mwaka. Vile vile Wizara itawasomesha wakulima 2,000 pamoja na wanafunzi 135 wanaogharamiwa na wafadhili wa nje.

**Sherehe za wakulima (NaneNane)**

70. Mheshimiwa Spika, mwaka huu ni mwaka wa tano tangu maonyesho ya Sikukuu ya Wakulima yaanzishwe. Sikukuu ya Wakulima inasaidia kuwaelimisha wakulima kuhusu kilimo na ufugaji bora kwa kujifunza kwa vitendo kutoka kwa wakulima na wafugaji wengine. Vile vile wakulima hupata fursa ya kuona bidhaa na teknolojia mpya zilizopo katika soko. Hivi sasa Chama cha Wakulima (TASO) na wakulima wenyewe wako kwenye maandalizi ya Sikukuu ya Wakulima ambayo kwa mara ya tatu mfululizo yatafanyika kitaifa mkoani Arusha. Kutokana na uhaba wa fedha za kujengea mabanda mikoa mingine imependekezwa maonyesho yafanyike Arusha ambako kuna uwanja wa kudumu wenye huduma muhimu. Wizara imeagiza uongozi wa TASO uwashirikishe wakulima wengi zaidi ili washiriki katika maonyesho haya kwa faida ya kueneza utaalamu wowote ule kwa wenzao ambao watakuwa hawakupata nafasi ya kujionea maendeleo mapya katika maonyesho hayo.

**Maendeleo ya Ushirika**

71. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ushirika Serikali inatambua umuhimu wa Vyama vya Ushirika kwa maendeleo ya wananchi. Hivyo katika kipindi cha mwaka 1997/98 itaendelea kuboresha mazingira ya utekelezaji wa sera na sheria ili Vyama vya Ushirika viweze kustawi na kuwakomboa wanachama wake kiuchumi na kijamii kadiri ya malengo ya sheria ya Ushirika ya 1991, pamoja na marekebisho ya sheria hiyo ya 1997. Aidha Wizara yangu itaendelea kutoa elimu, ukaguzi na mafunzo ya ushirika kwa wanachama, halmashauri na watendaji. Mkazo zaidi utawekwa kwenye ngazi ya Vyama vya Msingi, ambavyo ni kitovu cha Ushirika.

72. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itasimamia marekebisho ya Sheria ya Ushirika ya mwaka 1991 na kuhakikisha mahesabu ya kila chama yanakwenda na wakati, kwa kukaguliwa mara kwa mara na kuhakikisha mahesabu yanafungwa na kukaguliwa. Utaratibu huu utawapa nafasi wanachama kuyajadili mahesabu hayo na kuyatolea maamuzi. Katika kipindi cha 1997/98 kila Chama cha Ushirika itabidi kiwe na kamati ya elimu kwa madhumuni ya kuimarisha elimu kwa watumishi, Halmashauri na wanachama wa ushirika pamoja na kuendeleza elimu ya ushirika kwa umma. Kuimarika kwa elimu kutafanya wananchi waufahamu zaidi Ushirika na misingi yake pamoja na faida zake.

73. Mheshimiwa Spika, baada ya ajira ya Wakaguzi wa Ushirika kuhamishiwa Serikali Kuu, vile vile kuanzishwa kwa Mfuko wa Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika utakaochangiwa na Serikali na Vyama vyenyewe, Wizara imepata uwezo zaidi wa kusimamia utekelezaji wa sheria ya ushirika. Hivyo, kuanzia mwaka 1997/98 Wizara yangu ina mategemeo makubwa ya kubadilisha hali ya Ushirika.

**Marekebisho ya Muundo wa Wizara ya Kilimo na Mashirika ya Umma**

74. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1997/98 Wizara itaendelea kuzifanyia marekebisho sheria zinazohusu sekta ya kilimo na mifugo ili kuipatia sekta binafsi mazingira mazuri ya kushiriki katika utekelezaji wa shughuli zilizoachwa na Serikali. Aidha kwa upande wa Mashirika ya Umma, Wizara itaendelea kufanya marekebisho na ubinafsishaji, mwelekeo ni kubaki na Bodi za kusimamia na kudhibiti ubora wa mazao mbalimbali kwa niaba ya Serikali. Vile vile kubinafsisha shughuli zote zilizokuwa chini ya Bodi hizi ili ziendeshwe kibiashara. Wizara itaendelea kuwahamasisha washiriki (stakeholders) katika sekta ya kilimo na mifugo kuunda vikundi mbalimbali kulingana na mazao au shughuli inayowahusu. Juhudi za kuanzisha mifuko maalum ya kuendesha shughuli muhimu kama vile utafiti, huduma za kitalaam, na pembejeo zitaendelezwa.

**Utekelezaji wa Sera na Mipango ya Kilimo na Ushirika**

75. Mheshimiwa Spika, Sera Mpya ya Kilimo na Mifugo na Sera ya Ushirika zimekamilika na zimepitishwa na Serikali. Wizara hivi sasa inatayarisha mikakati ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu pamoja na programu ya kutekeleza sera hizo. Mara tu mikakati itakapokamilika nakala zitasambazawa kwa Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa na Wilaya na wahusika wote (stakeholders) katika sekta ya kilimo, mifugo na ushirika. Katika kipindi cha 1997/98 Wizara yangu itaendelea kutekeleza sera za Serikali za kijumla za uchumi na za sekta, kwa kuzingatia sera ya kuihusisha sekta binafsi na kuweka mazingira yenye kuvutia ili iweze kuwekeza katika kilimo na mifugo, Wizara yangu itaendelea kuimarisha na kuboresha majukumu muhimu yafuatayo:

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera za Sekta za Kilimo, Mifugo pamoja na Sera ya Ushirika nchini.

(b) Kuandaa utayarishaji wa programu ya muda wa kati ya uwekezaji katika sekta ya kilimo (Agricultural Sector Investment Programme) jukumu ambalo halikutekelezwa katika kipindi kilichopita cha 1996/97.

(c) Kuendeleza na kuimarisha huduma za ushauri, utafiti na mafunzo ya kitaalam kwa wakulima na wafugaji.

(d) Kuihusisha kikamilifu sekta binafsi katika utoaji wa huduma mbalimbali za kilimo na mifugo ili kuipunguzia Serikali mzigo katika utoaji huduma hizo.

(e) Kuendelea kushirikiana na Tume ya Rais ya kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) katika zoezi linaloendelea la kuangalia upya miundo ya mashirika na ubinafsishaji wake.

(f) Kuimarisha masoko na kufungua minada ya mazao na mifugo vijijini na mipakani ili kuratibu na kutathmini shughuli za sekta binafsi katika ununuzi wa mazao na pembejeo.

(g) Kuhamasisha uanzishaji wa Vyama vya Ushirika vya aina mbalimbali, pamoja na kuhakikisha ukaguzi wa mahesabu ya vyama unafanyika mara kwa mara.

(h) Kuimarisha ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu na taarifa muhimu za kilimo, mifugo na ushirika.

**Maendeleo ya Watumishi**

76. Mheshimiwa Spika, Wizara inatilia maanani sana umuhimu wa Watumishi kuwa na mazingira mazuri ya utendaji kazi**.** Hatuna budi kuzisimamia na kuzilinda haki zao ili waweze kufanya kazi kwa juhudi na uwezo wao mkubwa walionao. Napenda kuwashukuru watumishi wote wa Wizara ambao wamejitahidi kufanya kazi katika mazingira magumu na bado wakawa wavumilivu. Tunajitahidi kuyamaliza matatizo yote sugu katika kipindi hiki cha mwaka huu wa fedha. Kama yatabaki, basi yawe ni yale tu ya utendaji wa hapa na pale.

77. Mheshimiwa Spika, kazi kubwa tutakayoifanya mwaka huu ni maandalizi ya mpango wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa ajili ya watumishi waliobakizwa Wizarani. Lengo la mafunzo haya ni kuinua viwango vya ujuzi ili kuboresha utendaji wao wa kazi. Aidha tunatazamia kupandisha vyeo watumishi 1224 wa Kada mbali mbal.**IV. SHUKRANI**

78. Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuzishukuru nchi na mashirika mbalimbali ya kimataifa yanayoendelea kutusaidia katika juhudi zetu za kuendeleza kilimo, mifugo na ushirika nchini. Shukrani zetu ziwaendee wahisani wafuatao; wa kwanza ni nchi za Australia, Canada, China, Denmark, Finland, India, Indonesia, Ireland, Italia, Japan, Korea kaskazini, Marekani, New Zealand, Norway, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi, Sweden na Thailand. Na pili ni Mashirika na Taasisi za Kimataifa hasa; Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, UNDP, FAO, EU, UNICEF, SADC, WFP, IFAD, CFTC, CILCA, CIMMYT, EADB, HPI, ICRAF, ICRISAT, IDRC, IITA, ILCA, Sasakawa Global 2000. Ni dhahiri bado tunahitaji misaada yao ili tuweze kujenga msingi wa kujitegemea.

79. Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kutumia nafasi hii kutoa shukrani kwa wakulima na wafugaji wote nchini kwa kukubali kupokea mbinu mpya za uzalishaji wa mazao na mifugo wanayopelekewa na wataalam. Aidha napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao katika kipindi cha 1996/97 ambayo imewezesha Wizara yangu kutekeleza mambo mengi kwa ufanisi mkubwa kwa nia ya kuwaendeleza wakulima na wafugaji nchini. Vile vile napenda kuwashukuru Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Njelu Kasaka na Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Ushirika Luteni Kanali Tirumanywa Philibert Magere pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika yote yaliyo chini ya Wizara yangu kwa kazi nzuri waliyofanya pamoja na hali ngumu waliyo kumbana nayo katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kutokana na ufinyu wa bajeti katika kipindi cha 1996/97. Aidha napenda kumshukuru Ndugu Raphael Mollel aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu kwa kazi nzuri aliyofanya kwa kipindi cha miezi 18 tuliyokaa naye Wizarani. Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kazi ya kuchapa hotuba hii.

## V. MAOMBI YA FEDHA

80. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya sasa ninakaribisha ushauri, maoni na maelekezo zaidi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ili yanisaidie katika utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 1997/98. Pia ninaomba Bunge lako tukufu sasa liidhinishe **shilingi milioni 13,016.9** kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na **shilingi milioni 5,334.7** kwa ajili ya matumizi ya shughuli za maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo, shilingi milioni 560 ni fedha za hapa na **shilingi milioni 4,774.7** ni fedha za nje.

81. Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge nawashukuru kwa kunisikiliza na kwa kunivumilia.

**82. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.**